# KATIBA YA MFUKO WA MAZISHI WA JUMUIA YA ARRAHMAN

## Utangulizi

Arrahman ni jumuia ambayo imesajiliwa rasmi tarehe 28 February 2013 chini ya sheria ya jumuia zisizo za kiserikali.

Kabla ya kusajiliwa ilikuwa na mfuko maalum wa mazishi.Hivyo kilichofanyika ni marekebisho ili ulingane na hali halisi ya wakati tulio nao.Kwa marekebisho hayo, jumuia itakuwa dhamana ya kushughulikia mazishi kuanzia pale taarifa ya kifo itakapopokelewa ikishirikiana na familia, itashughulika kwa kuwasiliana na Hospitali, Polisi na sehemu zote zitakazohusika mpaka maiti ipatikanwe na kuzikwa.

Kwa kuanzia jumuia itatumia mawakala wa makampuni ya mazishi ya kiislamu zilizopo Slough.Lengo la baadae, mara tutapokuwa na jengo letu/msikiti wetu, jumuia itaanzisha shughuli za kushughulikia maiti kuanzia mwanzo mpaka kumalizika shughuli za mazishi.

Jumuia itakuwa na kiongozi maalumu pamoja na wajumbe wasiopungua wane kusimamia shughuli nzima za mazishi pamoja na kushughulikia suala zima la misaada yas kijamii.

Baada ya utangulizi huo, ni muhimu kujua nani mwanachama hai na wajibu wake, wajibu wa mfuko na uongozi wa mfuko.

### I.Nani Mwanachama

a) Uwanachama kwenye mfuko huu ni wa hiyari, hata hivyo kwa wale wote watakaopenda kujiunga na mfuko lazima wawe waislamu, na wanaoishi Slough na vitongoji vyake.

b) Wawe na makaazi yanayofahamika na iwapo wana familia wajulikanwe.

c) Mwanachama atakuwa ni pamoja na mke na mume, watoto wote wenye umri usiozidi miaka 24 na ambao hawafanyi kazi.

d) Kwa zile familia zenye watoto wenye upungufu kimaumbile ambao hawawezi kufanya kazi au kujiajiri wenyewe hawa watahudumiwa na jumuia pindi udhuru wa kifo ukiwakuta.

e) Inapendekezwa kuwa wazee wawashawishi watoto wao walioolewa au ambao wanafanya kazi wajiandikishe kwenye mfuko na kushiriki kwenye shughuli za jumuia.

f) Mfuko utachangia mazishi ya mgeni na mwanachama ambaye kwa bahati amekuja kutembea kutoka nje ya nchi, hafanyi kazi ndani ya nchi na faradhi ya kifo imemkuta.

g) Kama inavyoeleza hapo juu (kifungu), katika familia wale wote walio na umri wa miaka zaidi ya 24 watawajibika kujiandikisha na kufuata sheria na taratibu za mfuko na za jumuia kwa ujumla.

h) Ikiwa mwanachama atafia Afrika wafiwa watapewa £1000 kama ubani.

i) Ikiwa mwanachama atafia nchi za Ulaya au Asia Jumuia italipa gharama za mazishi kwa mujibu wan chi husika au gharama ya kiwango cha standard rate (takriban £3000 kwa 2019) italipwa familia kwenda huko na kugharimia maziko au mfuko utamlipa funeral director husika wa maziko.

j) Mfuko hautoweza kuisafirisha maiti kutoka nchi moja kwenda nyengine ikiwa kiwango cha gharama kitazidi £3000 pamoja na kulipia gharama za maziko.

k) Iwapo msiba umetokea hapa nchini, mbali na Slough, Jumuia itashirikiana na jumuia za kiislamu za eneo hilo kukamilisha mazishi kwa kulip gharama zinazohusika.

l) Mfuko utalipa malipo nusu ya gharama za mazishi kwa miezi sita ya mwanzo mwanajumuia atapojiunga, vyenginevyo alipie gharama za miezi 6 kwa kuanzia

**II.Wajibu wa Mwanachama**

a) Kujiandikisha kuwa mwanachama itakuwa ni kwa kujaza fomu maalum ya jumuia itakayoonyesha orodha kamili ya familia yake.

b) Kulipa ada ya mwaka ya £180 au £15 kwa mwezi. Inapendekezwa kuwa malipo yawe kwa kila mwezi na moja kwa moja (Direct Debit).Vile vile anaweza kulipa kwa mwaka.

c) Ada kwa wale ambao hawana familia baada ya kujiandikisha watalipa ada ya £120 kwa mwaka au £10 kwa kila mwezi , pia watatumia njia iliotajwa hapo juu.

d) Kuhudhuria vikao vyote vitakavyoitishwa na jumuia vitakavyozungumzia masuala ya kuendeleza mfuko huo.

e) Kuwa tayari kusaidia shughuli zinazohusiana na kitengo hicho cha jumuia. Kama vile kusaidia usafiri pindi atakapoombwa ili kufanikisha shughuli za mazishi.

f) Kuwa tayari kutoa maoni ambayo anahisi yataboresha uendeshaji na usimamizi wa mfuko maalum wa mazishi.

g) Mwanachama analo jukumu la kuuarifu uongozi wa mfuko anapobadilisha makaazi yake au njia za mawasiliano.

**III.Kusita Kuwa Mwanachama**

a) Mwanachama wa mfuko anaweza kujitoa wakati wo wote kwa kuuarifu uongozi juu ya dhamira yake hiyo .

b) Pia mwanachama ataweza/au atakuwa amejitoa baada ya kukamilisha miezi mitatu mfululizo bila ya kulipa ada ya uanachama ya mfuko huo.

c) Mwanachama pia anaweza pia kujitoa iwapo hakuathirika na maamuzi ya uongozi kuhusu shughuli zinavyoendeshwa.Bali kabla ya kujitoa itabidi apelike malalamiko

kwa uongozi wa mfuko na iwapo hakuridhika na uamuzi wao atapeleka malalamiko hayo kwa uongozi wa jumuia kwa kusikilizwa na kutolewa uamuzi.

d) Mwanachama anayo haki kulalamika kwa kuwasiliana na viongozi pale anapohisi mfuko haukuchukuwa hatua muafaka pale msiba unapotokea/ulipotokea baada ya kuuarifu uongozi kuhusiana na msiba uongozi ukazembea kuwasiliana na taasisi zinazohusika kama vile Polisi,Hospitali na kadhalika.

e) Iwapo mwanachama amegharimia mwenyewe kuanzia hatua yo yote kuanzia kutoa taarifa ya kifo mpaka mazishi kumalizika, anayo haki ya kurejeshewa gharama hizo. Gharama zinazotarajiwa hapa ni kama vile kusafirisha maiti kutoka nyumbani kupelekwa hospitali na kadhalika, gharama hizo hazijumlishi gharama za matumizi ya nyumbani wakati wa msiba na zilizofanana.

**IV.Wajibu wa Uongozi wa Mfuko**

a) Kuweka kumbukumbu sahihi za majina za majina zikiwemo namba za simu za wanachama wote wa mfuko

b) Kuwasiliana na wanachama kwa kuitisha mkutano angalau mara moja kila baada ya miezi sita.

c) Kuwaandikia barua za ukumbusho wale wote watakaokuwa hawajalipa ada zao kwa muda wa miezi mitatu na kuwapa tarehe ya mwisho ya kufanya malipo.

d) Kushughulikia malalamiko yote yatakayoletwa na wanachama.

e) Kutoa taarifa ya maendeleo , na matatizo ya uendeshaji wa mfuko pamoja na uongozi wa jumuia kila baada ya miezi mitatu.

f) Kutayarisha ripoti ya mfuko wa mazishi ya mwaka ili iweze kuchanganywa na ripoti nyengine za jumuia za kujitolea.

**V.Wajibu wa Uongozi wa Jumuia**

a) Kupokea ripoti ya uendeshaji wa mfuko za miezi mitatu/sita na za mwaka.

b) Kuzijadili ripoti hizo na kueleza itakapobidi namna bora ya kuboresha huduma za mfuko huo.

c) Ikibidi iwapo uongozi utahisi kuwepo haja ya kuongezwa nguvu uongozi wa mfuko ili kuleta ufanisi Zaidi au imedhihirika kuwa baadhi ya wajumbe hawabebi majukumu yao vizuri, wanaweza kubadilisha uongozi huo kwa kushirikiana, na kuwaarifu wanachama juu ya uamuzi huo.

d) Viongozi wa shughuli za jumuia kwa kualikwa wanaweza kuhudhuria vikao vya mfuko.

e) Kuidhinisha ulipaji wa gharama za mazishi kwa kampuni, au taasisi iliyohusika au kwa familia iliyopata msiba, kwa gharama za kawaida (normal rate), kwa 2019 haizidi £3000.Ikiwa familia itapendelea kuzika kwa VIP rate italipia ada ya juu wenyewe.

f) Jumuia haitokopesha fedha za mfuko wa maziko kwa mtu ye yote.

g) Ikiwa kifo kitamkuta mmoja wa mwanajumuia wa Arrahman ambaya si mwanachama wa mfuko, uongozi wa jumuia unaweza kusaidia kutoa matangazo kwa njia mbali mbali ya kuomba michango kwa wanajumuia, wanachama na waislamu kwa ujumla, ikiwa familia itakubali jumuia kufanya hivyo.

h) Ikiwa kutafanyika mchango wo wote wa marehemu ambayo jumuia itakabidhiwa itauwasilisha kwa familia, wao wataamua ikiwa watapenda kiwango Fulani kuchangia mfuko wa maziko au mfuko wa jumuia wa kununua jingo au vyenginevyo.

i) Mfuko hautolipia VIP rate kwa kuwakopesha wafiwa, cheque ya malipo ya standard rate itatolewa.Nyongeza yo yote familia italipia wenyewe. Mfuko unaweza kuchukua

fedha taslimu (cash) kutoka kwa wahusika kwa kufanya cheque kwa niaba yao na kuzirejesha kwenye mfuko

**Katiba hii ni Hati Miliki ya Arrahman Community and Educational Trust** *©2019*

**Ukiwa una swali lo lote tafadhali tuma barua pepe; arrahmancet@gmail.com**